**SOLOMON** ni mmoja wa waanzilishi na mwanachama wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Kampuni ina leseni kama Dalali/ Wakala, Meneja wa Mfuko, na Mshauri wa Uwekezaji kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ambayo ni taasisi ya serikali, iliyoanzishwa na Sheria ya Bunge ili kusimamia masoko ya mitaji na dhamana.

SOLOMON ina leseni ya uwakala wa ununuzi na uuzaji wa Dhamana na hatifungani za Serikali kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BOT). SOLOMON Stockbrokers pia ni kampuni ya kuaminika na yenye ufanisi miongoni mwa wanachama wa jumuiya ya mawakala/madalali wa soko la hisa.

Tangu kusajiliwa kwake mwaka wa 1996, SOLOMON imepata uzoefu katika masoko ya fedha na kujenga uaminifu katika uimara wa kuwahudumia wateja wake katika aina mbalimbali za bidhaa, huduma, ushauri & mafunzo.

Nia njema za maadili ya biashara na kufuata kanuni za sheria zimechangia sana katika ukuaji wetu kuwa kampuni kuu ya upatanishi wa kwanza kwa wateja mbalimbali katika sekta ya fedha. Kwa kuzingatia kanuni hizi, tumeweza kujenga uaminifu mkubwa na wateja wetu na kushinda sifa nzuri katika soko.Tumejitahidi kuhakikisha kuwa tunafuata miongozo na sheria zinazotawala sekta ya fedha, na hivyo kujenga msingi imara wa ukuaji wa biashara yetu. Tunajivunia kuwa mshirika wa uaminifu kwa wateja wetu katika kutoa huduma za upatanishi wa hali ya juu.

Wateja wetu ni Taasisi, Makundi ya mifuko ya hifadhi ya jamii, Mawakala wa bima na Vikundi mbalimbali vya jamii pamoja na Watu binafsi, Familia na Wastaafu.



## Dhima Yetu

Kuboresha maisha kupitia utoaji fursa za uwekezaji wenye kuaminika na kufikia malengo ya kukuza uchumi binafsi kwa wateja wetu.

## Maono Yetu

Ni kuwa mtoaji bora wa huduma za udalali/ uwakala wa hisa Ndani na Nje ya Nchi.

## Misingi Yetu

- Ufanisi
- Utaalamu
- Uadilifu
- Uajibikaji

### Wakala Na Mtunza Hisa

Wasiliana nasi kupitia wakala wetu Benki ya CRDB katika matawi yake yote hapa Nchini na Nje ya Nchi.





## ELIMU YA UWEKEZAJI HISA

SOLOMON tunatoa pia fursa ya Elimu ya Uwekezaji kwa watu wenye nia ya dhati ya kufahamu kuhusu soko letu la mitaji na dhamana. Elimu hii itaelezea juu ya uwekezaji kwenye hisa, vipande na hatifungani.

Elimu itatolewa kwa Makundi yafuatayo:

a. Makampuni ya UMMA & watu binafsi
b. VICOBA & Vikundi vya wajasiriamali
c. Vikundi vyovyote (ikiwemo wastaafu / wanaokaribia kustaafu)

Jinsi ya Kushiriki:

- Jiunge kwenye kikundi cha watu wasiopungua kumi iwe kwenye kundi lolote tajwa hapo juu.
- Tuma maombi ofisini kwetu kupitia barua pepe wekeza@solomon.co.tz

Mahali
Popote kundi/jumuiya yenu itakapopendekeza, maadam kuwe penye mpangilio mzuri.

TAHADHARI
Epuka matapeli kwa kuzingatia namba za simu na anuani ya barua pepe iliyotolewa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi

*Reach | Access | Invest*

## Huduma Zetu

- Dalali wa Masoko ya Hisa
- Wasimamizi wa Mfuko
- Washauri wa Uwekezaji

## Bidhaa Zetu

### HISA

Hisa ni sehemu ya umiliki wa kampuni. SOLOMON Stockbrokers ni wakala wa soko la hisa la Dar es Salaam anayeunganisha wawekezaji ambao wako tayari kuuza na wawekezaji ambao wako tayari kununua hisa zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam. Soko la hisa la Dar es Salaam lina safu mbili za kuorodhesha kampuni zilizokusanya mitaji kwa umma.Safu hizo ni safu za soko kuu (Main Investment Market Segment- MIMS) Kwa ajili ya kampuni kubwa zenye mitaji mikubwa, historia ya utendaji na utoaji wa gawio kwa wanahisa; na safu za kukuza kampuni na Ujasiriamali (Enterprise Growth Market Segment – EGM) kwa kampuni zisizokidhi sifa za kuorodheshwa kwenye safu kuu - MIMS.

### DHAMANA YA UWEKEZAJI NA USIMAMIZI RASILIMALI TANZANIA (UTT)

Ni mpango wa usimamizi wa Mifuko ya Uwekezaji wa pamoja kutoka kwa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania. Kampuni ya UTT AMIS inasimamia Mifuko/Miradi sita ya uwekezaji wa pamoja. Zaidi ya hayo, UTT AMIS inatoa huduma ya usimamizi mali za kifedha zinazokidhi mahitaji maalum kwa wawekezaji binafsi wa kipato cha kati, cha juu pamoja na Taasisi.

Mifuko hii ni:

- Mfuko wa Umoja,
- Mfuko wa wekeza Maisha
- Mfuko wa Watoto
- Mfuko wa Jikimu
- Mfuko wa Ukwasi
- Mfuko wa Hati Fungani

### DHAMANA ZA SERIKALI

Hizi ni dhamana za muda mfupi zinazotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ambazo ziinatolewa kwa njia ya Minada inayofanyika mara mbili kwa mwezi kila siku ya jumatano ya kazi kupitia mchakato wa ushindani wa zabuni katika Soko.

Benki Kuu ya Tanzania (BOT) hutoa dhamana za Muda mfupi katika awamu nne (Ndani ya mwaka) zenye ukomavu kama ifuatavyo:

Dhamana ya siku 35
Dhamana ya siku 91
Dhamana ya siku 182
Dhamana ya siku 364

### HATIFUNGANI

Hatifungani ni dhamana za muda mrefu zinazokomaa zaidi ya mwaka mmoja. katika Soko la Msingi/Awali, Benki Kuu ya Tanzania (BOT) hutoa Hatifungani za Muda mrefu (mara mbili kwa mwezi), Hatifungani hizi pia zinapatikana kwenye soko la pili la Hisa la Dar-es-Salaam (DSE).

Benki Kuu ya Tanzania inatoa aina za ukomavu wa Hatifungani katika vipindi vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Hatifungani za miaka 2 | - | 7.60% |
| Hatifungani za miaka 5 | - | 8.6% |
| Hatifungani za miaka 7 | - | 9.48% |
| Hatifungani za miaka 10 | - | 10.25% |
| Hatifungani za miaka 15 | - | 11.15% |
| Hatifungani za miaka 20 | - | 12.10% |
| Hatifungani za miaka 25 | - | 12.56% |

@sstockbrokers
@sstockbrokers
+255 714 269090

PSSSF House Ground Floor. Samora Avenue
Morogoro Road. P. O. Box 77049,
Dar es Salaam, Tanzania
Email: solomonstockbrokers@solomon.co.tz
Phone: +255 22 2124495
Mobile: +255 764 269090
Website: www.solomon.co.tz

# SOLOMON Stockbrokers Limited

*Mwanachama wa Soko la Hisa la Dar-es-Salaam*



Reach | Access | Invest